

Chanjo (shots) ni moja wapo ya njia tunazo, kupambana na magonjwa ya COVID-19.



Ili kukomesha magonjwa haya, tunahitaji kutumia njia zote za kuzuia. Chanjo ni moja wapo ya njia bora zaidi ya kulinda afya yako na kuzuia magonjwa. Chanjo hufanya kazi na kinga asili ya mwili wako ili uwe tayari kupambana na virusi. Hatua zingine, kama kuvaa kinyago kinachofunika pua yako na mdomo na kukaa mbali miguu 6 kutoka kwa watu wengine ambao hauishi nao, pia kusaidia kuzuia kuenea kwa COVID-19.

Uchunguzi unaonyesha kuwa chanjo ya COVID-19 inafaa sana kukuzuia kukuambukiza COVID-19. Wataalam pia wanafikiria kuwa kupata chanjo ya COVID-19 inaweza kukusaidia kuzuia kutabanika hata ikiwa unapata COVID-19. Chanjo hizi haziwezi kukupa ugonjwa .



Chanjo ni salama. Mfumo wa usalama wa chanjo ya Merikani inahakikisha kuwa chanjo zote ziko salama iwezekanavyo. Chanjo zote za COVID-19 ambazo zinatumiwa zimepitia vipimo sawa vya usalama na kufikia viwango sawa na chanjo zingine zozote zimetumiwa kwa muda mrefu. Mfumo uliowekwa kote nchini ambayo inaruhusu CDC kuangalia maswali ya usalama na kuhakikisha kuwa chanjo zinakaa salama.



Aina tofauti za chanjo za COVID-19 zitapatikana. Chanjo nyingi hutolewa kwa sindano ya ayina mbili, moja kwa wakati na nafasi mbali mbali. Sindano ya kwanza inauandaa mwili wako. Sindano ya pili inapewa nyuma ya wiki tatu baadaye ili kuhakikisha una ulinzi kamili. Ikiwa umeambiwa unahitaji sindano mbili, hakikisha kwamba unapata zote mbili. Chanjo zinaweza kufanya kazi kwa njia tofauti, lakini aina zote za chanjo zitakusaidia kujikinga.



Chanjo zinaweza kusababisha uzaifu wa mwili wa watu wengine, maumivu ya misuli, kuhisi uchovu, au homa kali. Hari hizi zinamaanisha chanjo inafanya kazi kusaidia kufundisha mwili wako jinsi ya kupambana na COVID-19 ikiwa umekutana na magonjwa haya. Kwa watu wengi, hari hizi hazitadumu zaidi ya siku moja au mbili. **Kuwa na hari hizi haimaanishi kuwa una COVID-19.** Ikiwa una maswali juu ya afya yako baada ya kudungwa sindano, piga simu kwa daktari wako, muuguzi, au kliniki. Kama ilivyo na dawa yoyote, hari yako ikiwa mbaya zaidi, kama ugumu wa kupumua, shariti utafute msaada wa kiafya. Siyo kwamba jambo hili litatoka. Lakini ikiwa litajitokeza, piga simu 911 au nenda kwenye chumba cha dharura cha karibu.



Unapopata chanjo, wewe na mfanyakazi wako wa huduma ya afya wote mtahitaji kuvaa vinyago.

CDC inapendekeza kwamba wakati wa janga/magonjwa haya, watu huvaa kinyago kinachofunika pua na mdomo wanapowasiliana na wengine nje ya kaya zao, wanapokuwa katika vituo vya huduma za afya, na wanapopokea chanjo yoyote, pamoja na chanjo ya COVID-19.



Hata baada ya kupata chanjo yako, utahitaji kuendelea kuvaa kinyago kinachofunika pua yako na mdomo, kunawa mikono mara nyingi, na kukaa angalau/mbali miguu 6 mbali kutoka kwa watu wengine ambao hauishi nao. Hii inakupata wewe na wengine kinga bora kutokana na kuambukizwa virusi. Hivi sasa, wataalam hawajui chanjo hiyo itakulinda kwa muda gani, kwa hivyo ni wazo nzuri kuendelea kufuata miongozo kutoka kwa CDC na idara yako ya afya. **Tunajua pia sio kila mtu ataweza kupata chanjo mara moja, kwa hivyo bado ni muhimu kujilinda na wengine.**